Kantor Dakwah Sulay
Telp. 2414488 2410615, fax: 232,

# JINSI ILIVYOKUWA SWALA YA MTUME صلى الله عليه وسلم



Abdul- Aziz ibn abdillah ibn Baz Sheikh
Kimefasiriwa na
Sheikh: Sulayman A.S. Shaqssy

19010008

# Jinsi ilivyokuwa
## Swala ya
## Mtume ﷺ

Kimetungwa na :
Shekh: Abdul-Aziz ibn Abdillah ibn Baz

kimefasiriwa na
Sheikh Sulayman A.S. Shaqssy

Mchapishaji na mtangazaji ni:
Ofisi ya uchapishaji na utafiti wa kielimu

Wizara ya mambo ya kiislamu na waqfu
na daawa na maelekezo

**1433 H**

ح) وزارة الشؤون الإسلامية والأوقاف والدعوة والإرشاد ، ١٤٢٥هـ

فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر

ابن باز ، عبدالعزيز بن عبدالله

كيفية صلاة النبي صلي الله عليه وسلم. / عبدالعزيز بن عبدالله ابن باز .- الرياض ، ١٤٢٥هـ

.. ص ؛ .. سم

ردمك : ٠-٨٧-٤٨٧-٢٩-٩٩٦٠

(النص باللغة السواحلية)

١- الصلاة أ. العنوان

ديوي ٢٥٢,٢     ١٤٢٥/٦٠٠٠

رقم الإيداع : ١٤٢٥/٦٠٠٠

ردمك : ٠-٨٧-٤٨٧-٢٩-٩٩٦٠

الطبعة الثانية

١٤٣٣هـ

## JINSI ILIVYO KUWA SWALA YA MTUME ﷺ

Kutoka kwa Abdul-Aziz Ibnu abdullaah Ibn baaz yamfikie kila mwenye kupenda kusali kama alivyo kuwa akisali Mtume ﷺ.

Na hayo ni kwa mujibu wa kauli yake ﷺ **"Salini kama mlivyo niona nasali"** (*bukhari*)

1. **Atawadhe vyema**, yaani atwadhe kama ilivyo amrishwa na Allah na kuitekeleza kauli yake (s.w):

قال تعالـــى:

﴿ يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا قُمْتُمْ إِلَى ٱلصَّلَوٰةِ فَٱغْسِلُواْ وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى ٱلْمَرَافِقِ وَٱمْسَحُواْ بِرُءُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى ٱلْكَعْبَيْنِ ﴾ [6: 5].

**Yaani:**

"Enyi mlio amini! Mnapo simama ili mkasli, basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa

vyenu,na (osheni) miguu yenu mpaka vifundonni" (5 :6)

Na pia kauli ya Mtume ﷺ:

"لا تقبل صلاة بغير طهور"

**"Swala haikubaliwi pasina udhu"**

2. **Anae Sali aelekee Qibla,** nayo ni al-kaaba.

Napopote awapo inamlazimu aelekee qibla kwa mwiliwake wote na akusudie kwa moyo wake kuiswali hiyo swala aitakayo: iwe ni faradhi au sunnah,na wala asiitamke nia kwa ulimi wake, kwa vile kuitamka kwa ulimi si jambo lililothibiti katika sheria,na Mtume ﷺ na maswahaba wake hawakuwa wakiitamka nia.

**Na** ni sunna kujiwekea **sutra** (kizuizi) pahala pa kuswalia, asalipo kama imamuau peke yake na hilo limeamrishwa na Mtume ﷺ. kuelekea qibla nisharti katika swala

ispokuwa katika sehemu fulanifulani zilizo tajwa katika vitabu vya masheikh.

3. **Apige Takbiratul-Ihram kwa** kusema :

"الله أكبـــر".

***Allaahu Akbar***

Hali macho yake yanaangalia mahali pa kusujudu.

4. **Ainue mikono yake** hadi usawa wa mabega au masikio yake.

5. **aikunje mikono yake kifuani,** wa kulia juu ya wa kushoto kama yalivyo kuja hayo katika hadithi ya wail-ibn hujr na qubaisa ibn halab at-tay kutoka kwa baba yake (r.a)

6. **Ni snna kusoma Duaul-istiftaah (*dua ya kuanzia swala*):**

"اللهم باعد بيني وبين خطياي كما باعدت بين المشرق والمغرب,

اللهم نقني من خطاياي كما نقيت الثوب الأبيض من الدنس, اللهم اغسلني من خطاياي بالماء والثلج والبرد".

***Allahumma ba'id bainiy wabaina khatwaayaay kama baadta bainal-mashriq wal-maghrib. allahumma naqqiny min khatwaaayaay kama yunaqqa ath-thaubul-abyadhuminad-danasi. Allahumma aghsilniy min khatwaayaay bil-maai wath-thalji wal-baradi.***

**Yaani:** ewe mola wangu niweke mbali na makosa yangu kama ulivyoiweka mbali mashariki na magharibi, ewe mola wangu nisafishe kutokana na makosa yangu kama inavyo safishwa nguo nyeupe kutokana na uchafu, ewe mola wangu nioshe kutokana na makosa yangu kwa maji na theluji na baridi.

Na akipenda atasema badala ya maneno hayo:

"سبحانك اللهم وبحمدك وتبارك اسمك وتعالى جدك ولا إله غيرك".

***"Subhaanakal-lahumma wabihamdika***

***watabaaraka smuka wataalaa jadduka walaa ilaaha ghairuka".***

**Yaani:** umetakasika ewe mola wangu na sifanjema ni zako, na limeakata jina lako na umetukuka ufalme wako na hapana mola apasae kuabudiwa ila wewe.

**Kasha aseme:**

"أعوذ بالله من الشيطان الرجيم, بسم الله الرحمن الرحيم".

***"Audhu billaahi minasshaitwani rrjiim, bismil-lahi rrahmani rrahiim".***

**yaani:** "nataka hifadhi kwa mwenyezimungu kutokana na shetani alie laaniwa,".

"kwa jina la mwenyezi mungu mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo mwenye kuneemesha neema kubwakubwa".

kasha asome suratul-faatihah, kwani mtume ﷺ amesema:

"لا صلاة لمن لم يقرأ بفاتحة الكتاب".

**yaani:** hapana swala kwa asieisoma suratul-faatihah.

Na mwisho wa sura hiyo aseme: (آمين) yaani: ewe mola wetu kubali. aseme kwa sauti kama swala ni ya kusoma kwa sauti, na aseme kwa siri kama swala ni ya kusoma kwa siri, kisha asome anchokiweza katika qur`ani.

7. Arukuu huku akileta takbira na kunyanyuwa mikono yake usawa wa mabega yake au masikio, kichwa chake kinyanyuke usawa wa mgongo wake na mikono yake iwe juu ya magoti yake akiwa amevichanua vidole vyake, atulie katika rukuu yake na aseme (سبحان ربي العظيم) ***"subhaana rabbiyal-adhiim"*** yaan: "ametakasika mola wangu mtukufu na sifa zote za upungufu" ni bora zaidi ayakariri maneno hayo mara tatu au zaidi, pia ni bora zaidi aseme:

"سبحانك ربنا وبحمدك اللهم اغفر لي".

***Subhanakal-lahumma rabbana wa bihmdika allahumma ghfrly.***

**Yaani:**
Umetakasika ewe mola wangu, ewe mola wetu sifa njema zote ni zako, ewe mola wangu nighufirie (nisamehe).

8. Aanue kichwa kutoka rukuu, hali ameinua mikono yake usawa wa mabega yake au masikio yake huku akisema:

"سمع الله لمن حمده".

***"Sami-al-lahu limani hamidah".***

Yaani Mwenyezimungu anamsikia kila anaemsifu. ayaseme hayo akiwa imamu au peke yake na anapokua amesimama wima aseme:

"ربنا ولك الحمد حمداً كثيراً طيباً مباركاً فيه ملء السماوات
وملء الأرض وملء ما بينهما وملء ما شئت من شيء بعد".

***Rabbana wa lakal-hamd, hamdan kathira twayyiban mubarakan fihi mil`a s-samawti wa mil` a l-ardhi ,wa mil`a maa bainahumaa, wamil` a maashi'ta min shay"in ba"d.***

**Yaani:**

"ewe mola wetu! sifa njema na shukurani za dhati nizako. tunakusifu sifa nyingi njema na zenye baraka ujazo wa mbingu na ujazo wa ardhi na ujazo wa vilivyomo baina yake na ujazo wa chochote ukitakacho baada ya hivyo".

Na nisawa ukiongeza baada ya kusema hayo:

"أهل الثناء والمجد أحق ما قال العبد وكلنا لك عبد اللهم لا مانع لما أعطيت ولا معطي لما منعت ولا ينفع ذا الجد منك الجد".

***Ahlath-thanai wal-majd, ahaqqu ma qalal-abdu, wa kulluna laka abdu allahumma laa mani" a limaa Atwyita walaa mu" twiya limaa mana" ta walaa***

***yanfa" u dhal jaddi minkal-jaddu.***

**Yaani:**

"Wewe ndiye mwenye kusitaki kusifiwa na kutukuzwa. Yaliyo kweli zaidi ni yale ayasemayo mja katika kukusifu wewe nasi sote niwaja wako. Ewe mola wangu! hamna wakuzuwia ulicho towa, na hapana wakutoa ulichozuia, wala tajiri hautamfaa utajiri wake mbele yako".

hayo yamethibiti katika baadhi ya hadithi sahihi za mtme ﷺ Lakini akiwa ni mamuma basi katika katika kuinuka kutoka rukuu atsema:

"ربنا ولك الحمد".

***Rabbana walakali hamd...***

**Yaani:**

Ewe mola wetu sifa njema zote ni zako... hadi mwisho kama ilivyo tangulia. Naiyiweke mikono yake juu ya kifua chake kama alivyo fanya katika kusimama kwake kabla ya kurukuu kama yalivyothibiti hayo

kwa mtume ﷺ katika hadithi ya Wail ibn hujri na Sahl ibn Sa"d (r.a)

9. Asujudu huku analeta takir akiwa ameyatanguliza magoti yake kabla ya mikono, ikwa hilo ni jeoesi kwake, la sivyo atatanguliza magoti kabla ya mikono yake na vidole vya miguu yake vielekee qibla, na vidole vya mikono yake vigusane baala ya kuvichanua na awe ju ya viungo vyake saba: paji la uso na pua, mikono miwili na magoti mawili na matumbo ya vidole vyake vya miguu na aseme:

"سبحان ربي الأعلى".

***Subhana rabbiyal-a"alaa***

**Yaani:** mola wangu ametakasika na sifa zote za upungufu. akariri tasbihi hiyo mara tatu au zaidi. Ni vizuri pamoja natasbihi hiyo aseme.

"سبحانك ربنا وبحمدك اللهم اغفر لي".

***Subhanaka allahumma rabbana wabhmdika allahumma ighifirly.***

**Yaani:** umetakasika ewe mola wangu na sifa njema zote nizako! ewe mola wangu nisamehe.

Naakithirishe dua kwa vile mtume ﷺ amesema:

"أما الركوع فعظموا فيه الرب وأما السجود فاجتهدوا في الدعاء فقمن أن يستجاب لكم".

**Yaani:**
"Ama katika rukuu muadhimisheni mola wenu, na katika sijda basi jitahidini kwa dua kwani dua zenu katika sijda nizenye kuelekea zaidi kwenye kujibiwa". (*muslim*)

Na kauli yake ﷺ mja huwa yu karibu zaidi na mola wake katika sajida basi zidisheni sana dua. (*muslim*)

Yatakikana muislamu ajiombee kwa mola wake na awombee wenziwe miongoni mwa waislamu kheri za dunia na akhera katika salah za faradhi na sunna.

Katika kusujudu aiepushe mikono yake mbali na mbavu zake na mapaja yake mbali na miguu yake na mikono yake kati ya viganja na vifundo isiguse chini kwani mtume ﷺ amesema: nyookeni katika sajda na msiilaze mikono yenu chini kama ailazavyo mbwa.

10.Ainue kichwa chake kutoka katika sijda kwa takbir

"الله أكبـــر".

*"Alahu akbar"* na akae juu ya mguu wake wa kushoto hali amesimamaisha **mguu** wake wa kulia, na aiweke mikono yake juu ya mapaja yake karibu na magoti yake na hapo aseme:

"رب اغفر لي، رب اغفر لي اللهم اغفر لي، اللـــهم اغفـــر لي وارحمني وارزقني وعافني واهدني واجبرني".

***Rabbighfrly rabbighifrly, rabbighfirly allahumma ghffirly warhamny warzuqny waafiny wahdiny wajburny.***

**Yaani:**

Ewe mola wangu nisamehe, ewe mola nisamehe, ewe mola nisamehe ewe mola wangu nisamehe, nihurumiye, niruzuku, nijaalie afya, niongoze na nitengenezee yaliyoniharibikia.

"Atulie katika kukaa kwake mpaka kila kiungo kirudie mahali pake kulingamana kwake katika it" dali baada ya rukuu, na hayo nikwa vile mtume ﷺ alikuwa akirefusha kutulia kwake baada ya kurukuu na baina ya sajida mbili.

11. Asujudu sijda ya pili kwa takbir, na afanye yale aliyo yafanya katika sajida ya mwanzo.

12. Ainuke kutoka katika sijda kwa takbir na akae kikao hafifu kama alivyo kaa baina ya sajida mbili, na hi yaitwa "jalistul-istirahah" (kikao cha mapumziko), nacho ni mustahabu (kinapendeza) kwa mujibu wa kauli sahihi miongoni mwa kauli za ulamaa, na akiacha sineno, wala hamna ndani yake

dhikri wala dua kisha ainuke wima, kuiendea rakaa ya pili: ainuke kwa kujisukuma juu ya magoti yake kama akiweza, ama ajitegemaze juu ya ardhi asipoweza, kisha asome suratul fatihah na chochote kilicho chepesi kwake katika qur'an baada ya hiyo al-fatihah, kisha afanye yale yote aliyoyafanya katika rakaa ya kwanza.

Haijuzu kwa ma`muma kumtangulia imamu wake katika salah, kwani mtume ﷺ ametahadharisha dhidi ya jambo hilo; na nimakruhu kwenda naye sambamba katika matendo ya salah, lililo sunna nikuwa matendo yake (maamuma) yote ayaletwe: kila tendo baada ya tendo la imamu bila ya uvivu, na aanze kumfuatiliza baada ya kukatika sauti ya imamu ya kuashiriya tendo hilo na hayo nikwa mujibu wa kauli ya mtume ﷺ.

"إنما جعل الإمام ليؤتم به فلا تختلفوا عليه فإذ ا كبّر فكبروا وإذا قال سمع الله لمن حمده فقولوا ربنا ولك الحمد فإذا سجد فاسجدوا"

(متفق عليه).

**Yaani:**

"Hakika amekuwepo imamu ili afuatwe, basi musimukhalifu na akisema allahu akbar nanyi semeni alllahu akbar (wala msiseme: allahu kabar mpaka amemaliza kusema allah akbar) Na akisema: sami al-lahu limani hamdah semeni: rabbana walakal`hamdu (wala msiseme hayo mpaka amemaliza kusema: sami-allahu limani hamdah) Na akisha sujudu nanyi sujuduni (bukhari, muslim).

13. Salah ikiwa nirakaa mbili kama salah ya alfajiri, ijuma au idd, akae baada yakuinuka kutoka katika sijda ya pili juu ya mguu wake wa kushoto hali ya.

kuusimamamaisha mguu wake wakulia huku ameweka mkono wake wakulia juu ya paja lake la kulia, hali amevikunja vidole vyake isipokua kidole chake cha shahada atakachoashiria tawhidi. Napia ni vyema kama akivikunja vidole viwili: kidogo kabisa na cha pete huku akiweka kidole gumba juu

ya kidole cha kati; na akitumie kidole chake cha shahada kuonyesha ishara ya tawhidi na hayo yote yamethibiti kufunywa na mtume ﷺ. Na ni bora kwake kufanya aina hii wakati mmoja na aina ile wakati mwengine. Naaweke mkono wake wakushoto juu ya paja la kushoto karibu na goti lake, na hapo asome tashahhud katika kikao hicho.

"التحيات لله، والصلوات، والطيبات، السلام عليك أيها النبي ورحمة الله وبركاته السلام علينا وعلى عباد الله الصالحين أشهد أن لا إله إلا الله وأشهد أن محمداً عبده ورسوله".

***Attahiyyatu lillaah,was-swalawaatu wat-twaiyyibaatu. Assalamu alayka ayyuhan-Nabiyyu wa rahmatul-Lahi wabarakaatuh. Assalamu alayna wa 'ala ibaadil-Laahis-swaalihina.Ash-hadu an laa ilaaha illal-Laah,wa ash-hadu anna Muhammadan abduhu wa Rasuuluh .***

**Yaani:**

"Taadhima zote zinamstahiki Mwenyezi Mungu, vilevile rehma na mazuri yote

hutupatia Mwenyezi Mungu. Amani ya Mwenyezi Mungu ikuteremkie ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu pamoja na rehma na baraka zake. Nasi pia itushukie amni ya Mwenyezi Mungu pamoja na waja wake wema wote. Nakiri kuwa hakuna Mola ila Mwenyezimungu, na nakiri kuwa Muhammad ni mja wake na ni Mjumbe wake".

Kisha aseme:-

"اللهم صلّ على محمد, وعلى آل محمد, كما صـــليت علـــى إبراهيم, وآل إبراهيم، إنك حميد مجيد, وبارك على محمد, وعلى آل محمد, كما باركت على إبراهيم, وعلى آل إبر اهيم, إنـــك حميـــد مجيد".

***Allahumma swalli 'ala Muhmmad,wa ala aali Muhammad, kamaa swal-layta alaa Ibraahima wa ali ibrahima innaka hamidun Majidun. Wabaarik 'ala Muhammadin wa 'ala aali Muhammadin kama baarakta 'ala Ibraahima wa ali ibraahima, Innaka hamiidun Majiidun.***

**Yaani:**

"Ewe Mwenyezimungu! mrehmu Mjumbe wako Muhammadi na wafuasi wake nabii Muhammadi, kama ulivyo mrehemu Nabii Ibrahiim na wafuasi wake Nabii Ibrahiim. Wewe ndiye unaye stahiki kusifiwa na viumbe vyote na ndiye Mwenye Utukufu. Na umbariki nabii Muhammadi na wafuasi wake Nabii Muhammadi, kama ulivyo mbariki nabii Ibraahim na wafuasi wake Nabii Ibrahiim.wewe ndiye unayestahiki kusifiwa na viumbe vyote, na ndiye Mwenye Utukufu".

Na aombe hifadhi kwa Mwenyezi Mungu kutokana na mambo manne kwa kusema:-

"اللهم إني أعوذ بك من عذاب جهنم، ومن عذاب القبر، ومن فتنة المحيا، والممات، ومن فتنة المسيح الدجال".

***Allahumma inny a'udhu Bika min'ahdbi jhannam, wa mina adhaabil-qabri, wa min fitnatil-mahya, wal-mamaati, wamin fitnatil-masiihid-Dajaal.***

**Yaani:**

"Ewe Mola wangu! mimi ninajilinda kwako kutokana na adhabu ya Jahan-nam, na kutokana na adhabu ya kaburi, na kutokana na fitna ya uhai na mauti, na kutokana na fitna ya Masihid-Dajjaali".

Kisha aombe apendacho miongoni mwa kheri za dunia na Akhera. Na akiwaombea wazazi wake na waislamu wengine ni sawa .Iwe ni swala ya faradhi au ya sunnah. Kisha atoe salamu kuliani na kushotoni kwa kusema;-

"السلام عليكم ورحمة الله"

"السلام عليكم ورحمة الله"

***Assalamu alaikum warahmatullaah.***
***Assalamu alaikum warahmatullaah.***

14. **Sala ikiwa ni rakaa tatu** kama Maghribi, au nirakaa nne kama Adhuhuri, Alasiri au Isha, basi asome tashah-hudi kama tulivyo tangulia kuitaja pamoja na kumsalia Mtume ﷺ, kisha asimame wima na katika

kuinuka autegemeze uzito wa mwili wake juu ya magoti yake, ainue mikono usawa wa mabega yake hali ya kusema:-

***Allaahu akbar.***

"الله أكبر".

Hapo aikunje mikono yake juu ya kifua chake kama ilivyo tangulia, na asome suuratul-Faatihah peke yake.

Na kama baadh ya nyakati akisoma baada ya suurattil-Faatiha sehsmu ya Qur-ani, basi hamna neon kwa kuthibiti kuwa Mtume ﷺ nae alikuwa akifanya hivyo, na hayo yamo katika hadithi ya Abuu saiidi (r.a). Kisha asome tashah-hudi baada ya rakaa ya tatu katika sala ya Magharibi, na ya nne katika Adhuhuri, Alasiri na Isha, na amsalie mtume ﷺ na aombe hifadhi kwa Mwenyezimungu kutokana na Adhabu ya jahan-namu, adhabu ya kaburi na Fitna ya masihid-Dajjaali. Na akithirishe dua kama tulivyo tangulia kusema katika sala ya rakaa mbili.

Lakini katika kikao hiki cha Tashahudi ya mwisho akae kwa njia ambayo mguu wake wa kushoto uwe chini ya mguu wa kulia, na tako lake juu ya ardhi huku mguu wake wa kulia umesimama, na hayo ni kwa mujibu wa hadithi ya abuu Hamid (r.a), kisha atoe salamu kuliani na kushotoni kwa kusema:-

***Assalamu alaykum warahmatul-laah.***
***Assalamu alaikum warahmatul-laah.***

"السلام عليكم ورحمة الله".

"السلام عليكم ورحمة الله".

Hapo alete istighfari mara tatu na aseme:

"اللهم أنت السلام ومنك السلام، تباركت يا ذا الجلال والإكرام، لا إله إلا الله وحده لا شريك له، له الملك وله الحمد وهو على كل شيء قدير، اللهم لا مانع لما أعطيت، ولا معطي لما منعت، ولا ينفع ذا الجد منك الجد، لا حول ولا قوة إلا بالله، لا إله إلا الله ولا نعبد إلا إياه، له النعمة وله الفضل وله الثناء الحسن، لا إله إلا الله، مخلصين له الدين ولو كره الكافرون".

***Allahumma antas-salaamu,wa minkas-***

***salaamu, tabaarakta yaadhal-jalaali wal-ikraami. Laa ilaaha illal-laahu wahdahu laasharika lahu, lahul-Mulku, walahul-hamdu, wa Huwa alaa kulli shai-in qadiir. Allahumma laa mania limaa a-atwaita, wala mu-uutwiya limaa manaata wala yanfau dhal-jad-di Minkal-jaddu. Laa haula walaa quw-wata illaa bil-laahi. Laailaaha illal-laahu walaa naabudu illaa iy-yaahu, lahun-niimata, walahul-fadhlu, walahuth-thanaaul-hasan. Laailaaha illal-laahu, much-liswiina lahud-diina walau karihal-kaafiruun.***

**Yaani:**

"Ewe mola! wewe ndie amni. na Amani yatokana na wewe. Ume tukuka Ewe Mwenye utukufu na na kutukuza. hapana Mola anye stahiki kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu, peke yake hana mshirika. Ufalme ni Wake na Sifa njema zote ni zake. Naye ni mwenye uwezo juu ya kila kitu. Ewe Mola! Hapana wa kuzuiaUlicho toa, wala wa kutoa ulicho zuia, wala tajiri hautamfaa utajiri

wake mbele yako. Hapana hila wala uwzo ila utokane na Mwenyezi Mungu. Hapana Mola anyestahiki kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu. Nasi wala hatumuabudu ila yeye. Neema ni zake, fadhila na sifa njema zote pia ni zake. Hapana Mola anyestahiki kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu, nasi tumemtakasia dini yeye peke yake hata makafiri wakichukia".

Kisha amsabihi MwenyeziMungu kwa kusema:-

"سبحان الله".

***Subhaanal-Llaah***

**Yaani:**

"Ametakata Allaah" mara thalathini na tatu, na amhimidi Alla hmara thalathini na tatu kwa kusema:

"الحمد لله"

***Al-hamdu lil-Laah***

**Yaani:** Sifa njema zote ni za Allah, na amkabbir Allah mara thalathini na tatu kwa

kusema:

"الله أكبـــر"

*Allahu Akbar*

**Yaani:** "Mwenyezi Mungu ndiye mkubwa kuliko wote", na kwa kukamilisha aseme:

"لا إله إلا الله وحده لا شريك له, له الملك وله الحمد, وهـــو على كل شيء قدير".

***La ilaaha illal-Lahu Wahdahu la sharika lahu, Lahul-Mulku wa Lahul-hamdu wahuwa alaa kulii shay-in Qadir.***

Pia asome Ayatul-kursiyyu:

﴿ ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلْحَىُّ ٱلْقَيُّومُ ۚ لَا تَأْخُذُهُۥ سِنَةٌ وَلَا نَوْمٌ ۚ لَّهُۥ مَا فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِى ٱلْأَرْضِ ۗ مَن ذَا ٱلَّذِى يَشْفَعُ عِندَهُۥٓ إِلَّا بِإِذْنِهِۦ ۚ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ ۖ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَىْءٍ مِّنْ عِلْمِهِۦٓ إِلَّا بِمَا شَآءَ ۚ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ

ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ ۖ وَلَا يَـُٔودُهُۥ حِفْظُهُمَا ۚ وَهُوَ ٱلْعَلِيُّ

ٱلْعَظِيمُ ﴾ [2: 255].

***Allahu laa ilaha illa huwal-hayyul-qayyum. Laa ta"khudhuhu sinatun walaa nawm. lahuu maa fis-samawati wama fil-ardhi mandhalladhy yashfa'u indahu illaa bi'idhinihi. ya'alamu maa bain ayidihim wamaa akhalifahum, walaa yuhituna bishayin min ilmihi illa bimaa shaa'a wasi'a kursiy-yuhus-samaawaati wal-ardhi, walaa yau-uduhu hifdhuhuma wahuwal-aliy-yul-adhwiim.***

**Yaani:**

"Mwenyezi Mungu hakuna Mola ila yeye, (na) ndiye mwenye uhai wa milele, Msimamia kila jambo. Kusinzia hakumshiki wala kulala. Nivyake (peke yake vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo kwenye ardhi. Na nani huyo awezaye kuombea mbele yake (Mungu) bila ya idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yake (viumbe) na

yaliyo nyuma yao, wala (hao viumbe) hawalijui lolote katika yaliyo kwenye ilmu yake (Mwenye zi Mungu) ila kwa alipendalo mwenyewe. Enzi yake imeenea katika mbingu na ardhi, wala kuvilinda hivyo hakumshindi. Na yeye peke yake ndiye aliye juu na Ndiye aliye Mkuu." (2:255)

Pia asome Suratul-Ikhlas (sura ya 112) na Al-Muawidhwatain), suratul-Falaq na suratun-Naas (sura ya 113 na 114) baada ya kila swala. Ni mustahabu (inapendeza) zikaririwe hizi sura mara tatu tatu baada ya swalatul-Fajrina Al-Maghrib, kwa vile kuna hadithi sahihi ya Mtume ﷺ juu ya hilo. Napia ni Mustahabu alete ziada ya hio dhikri tuliyo itaja baada ya swalatil-Fajri na Al-Maghribi maneno yafuatayo mara kumi:

"لا إله إلا الله وحده لا شريك له, له الملك وله الحمد يحيي ويميت وهو على كل شيء قدير".

***Laa ilaaha illa llaahu wahdahu laa shariyka lahu lahul-mulku,walahul-hamdu,***

***yuhyii wayumiitu, wahuwa alaa kulli shaiy-in qadiir.***

**Yaani:**

"Hapana Mola anyestahiki kuabudiwa ila Allah, yeye peke yake hana mshirika. Ufalme niwake na pia sifa njema zote ni zake. Anahuisha na kufisha. Naye ni Muweza juu ya kila kitu".

Kama yeye ni imamu, basi baada ya salamu awaelekee watu, baada ya kuleta istighfari mara tatu na baada ya kusoma *"Allahumma Antas-salamu..."*

Kisha alete zile dhikri tulizo zitaja kama ambavyo zimeashiriwa katika hadithi nyingi za Mtume ﷺ, mojawapo ni ile Hadithi ya Bi Aisha (r.a) katika sahihi Muslim. Na adhkari zote hizi ni sunna wala si Faradhi. Na ni mustahabu kwa kila muislamu mume na mke achunge kuzisali rakaa 12 anapokuwa simsafiri, nazo ni: Nne kabla ya Ahuhuri, mbili baada ya Maghribi mbili baada ya Isha

na mbili kabla ya Al-fajri, hayo ni kwa vile Mtume ﷺ alikuwa akijitahidi sana kutozikosa sunna hizo ambazo zaitwa *A-rawaatib* na imethibiti katika sahihi M*uslim* hadithi iliyopokewa na Ummu habibah (r.a) kwamba Mtume ﷺ amesema:

"من صلى اثنى عشرة ركعة في يومه وليلته تطوعاً بنى الله له بيتاً في الجنة" (مسلم).

**Yaani:**

"Atakae swali rakaa kumi na mmbili katika usiku wake na mchana wa kw akhiyari ili amridhishe Mwnye zi Mungu, basi mola atjengea nyumba peponi" (*Muslim*)

Ama safarini, basi Mtume ﷺ alikuwa akiziacha suna za Adhuhuri, Maghribi na Isha, lakini akisali sunna ya swala a Al-fajri na Witri. Nayeye Mtume ﷺ ndiye kiigizo chetu chema kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w)

﴿لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ ٱللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ﴾[33: 21].

“Bila shaka mna mfano mwema (ruwaza nzuri) kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu” (33: 21)

Na Mtume ﷺ amesema :-

”صلّوا كما رأيتموني أ صلي“.

“Yaani salini kam mlivyo niona nasali.”

Na Mwenyezimungu ndiye mwenye kuwezesha na kuwafiksha.

Na sala na salamu zimshukie Nabii wetu Muhammadi ibn Abdil-llaahi na ahli zake na sahaba zake na wafuasi wake, na wote wenye kumfuata kwa utiifu hadi siku ya malipo.

**Aamin.**

# كيفية صلاة النبي
## صلى الله عليه وسلم

تأليف

## عبد العزيز بن عبد الله بن باز

باللغة السواحلية

وكالة المطبوعات و البحث العلمي
وزارة الشؤون الإسلامية والأوقاف والدعوة والإرشاد
المملكة العربية السعودية

١٤٣٣هـ

مكتب الدعوة بالسلي
هاتف ٢٤١٠٦١٥ ٠١ تحويله ٥٥٥ - ٢٤١٤٤٨٨ ٠١ ناسوخ ٢٣٢

السلي

# كيفية صلاة النبي

صلى الله عليه وسلم



تاليف / عبد العزيز بن عبد الله بن باز

ترجمة / سليمان شاكسي

الحساب الموحد بمصرف الراجحي SA 2280000296608010070509

السواحلية